



KKKT - DAYOSISI  
YA KUSINI

ELCT - SOUTHERN  
DIOCESE



## IGUMBILO GIRLS' SECONDARY SCHOOL

*Motto: Education is for prosperous life*

📍 Igumbilo Secondary School  
P.O. Box. 42 Chimala, Mbeya  
☎️ +255 769 051 665  
+255 756 279 304  
🌐 [igumbilogirls.ac.tz](mailto:igumbilogirls.ac.tz)  
✉️ [girlssecigumbilo@yahoo.com](mailto:girlssecigumbilo@yahoo.com)  
[info@igumbilogirls.ac.tz](mailto:info@igumbilogirls.ac.tz)

### PROGRAMU MAALUMU YA MAFUNZO YA AWALI KIDATO CHA KWANZA (PRE FORM ONE) 2024

Kozi maalumu ya kuwajengea msingi kidato cha kwanza 2025 itaanza tarehe **01/10/2024** mpaka tarehe

**20/12/2024**. Gharama ya kozi kwa muda wote ni **Tsh 200,000/= (Laki mbili tu)**

#### 1. MPANGO WA MASOMO

Mwanafunzi atafundishwa masomo yote ya sekondari kikamilifu.

#### 2. HUDUMA MBALIMBALI

##### • CHAKULA

Muda wote mwanafunzi awapo shuleni atahudumiwa chakula kwa ratiba hii: Uji saa 12:30 asubuhi, Chai pamoja na vitafunwa saa 4:10 asubuhi Chakula cha Mchana saa 8:35 mchana na Chakula cha jioni saa 12:00 jioni.

##### • AFYA

Mwanafunzi atapewa huduma ya kwanza endapo ataumwa, kama itahitajika matibabu zaidi atapelekwa hospitali na mzazi utajulishwa, Kwa mwenye bima za afya aje nayo.

#### 3. MAHITAJI YA KUJA NAYO SHULENI KWA MATUMIZI YA MWANAFUNZI

- ❖ Godoro ukubwa wa  $2\frac{1}{2} \times 6$
- ❖ Chandarua kimoja ni muhimu sana (kiwe cha Pembe nne)
- ❖ Sanduku la bati imara moja (TRANKA)
- ❖ Shuka 2 (rangi ya pinki moja na rangi ya bluu bahari moja)
- ❖ Viatu vyovyote, soksi nyeusi jozi nne
- ❖ Track suit ya Kijani mgomba yenye mistari myeupe
- ❖ T-shirt mbili zinapatikana shuleni uje na Tsh 30,000.
- ❖ Sare alizosomea shule ya msingi, nguo za ndani walau sita na nguo za nyumbani ndefu pea tatu.
- ❖ Peni, Penseli, Rula na Mkebe na daftari ndogo za msomi 12
- ❖ Vifaa vya usafi binafsi kama ndoo, mswaki, sabuni, taulo, ndala, sabuni za kuogea, mafuta ya kupakaa HATURUHUSI VIPODOZI NA MARASHI YOYOTE YENYE HARUFU KALI.
- ❖ Vifaa vya chakula kama sahani ya bati yenye mgawanyo ndani, kikombe cha bati na kijiko
- ❖ Fedha kidogo kwa matumizi ya mtoto. Fedha hiyo itatunzwa ofisi ya makamu mkuu wa shule na itatolewa kwa utaratibu uliopo.

-Mtihani wa kujiunga kidato cha kwanza utafanyika tarehe **21/09/2024**, awamu ya pili tarehe **28/09/2024** na awamu ya mwisho tarehe **5/10/2024** mwombaji anatakiwa kuchagua kati ya tarehe hizo.

-Malipo ya gharama ya kozi yalipwe kupitia benki ya **CRDB AC/NO 0152421086100** Jina la akaunti ni **IGUMBILO GIRLS' SECONDARY SCHOOL**, kisha risiti halisi (**Original Pay in Slip**) ya malipo iletwe shuleni siku ya kuripoti.

Kwa mawasiliano tumia namba hizi **0756279304** au **0769051665**

**KWA ELIMU NA MALEZI BORA SEKONDARI YA IGUMBILO NI CHAGUO LAKO**